# SINGIDA YETU

## NURU YA MAENDELEO

*JARIDA MAALUM LA OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA*

TOLEO LA DESEMBA **2025**

# RC DENDEGO NA SAFARI YA JIJI LA SINGIDA



**MHE. HALIMA DENDEGO**

*MKUU WA MKOA WA SINGIDA*



**Bima ya Afya kwa Wote:**

**"Mteja ni Mfalme"**



**DKT. FATUMA MGANGA**

*KATIBU TAWALA MKOA WA SINGIDA*

# UTANGULIZI

Toleo hili la Desemba 2025 linakuja kama hitimisho la mwaka uliobeba maamuzi, mageuzi na kasi mpya ya maendeleo katika Mkoa wa Singida. Ni toleo linalosimulia hadithi ya uongozi wa vitendo, mshikamano wa jamii, uwekezaji katika watu na rasilimali, pamoja na dhamira ya dhati ya Serikali ya Mkoa katika kujenga Singida salama, yenye uchumi imara na kizazi chenye maadili. Kupitia makala, taarifa maalum na matukio kwa picha, jarida hili linaakisi safari ya Singida kuelekea mustakabali unaong'aa kitaifa na kimataifa.

Toleo hili pia linaangazia juhudi za Mkoa katika mageuzi ya kidijitali kwa kuwajengea uwezo wajasiriamali kutumia mifumo ya kimataifa ya utambulisho wa bidhaa (GS1 Barcodes na QR Codes), hatua inayofungua milango ya masoko ya kitaifa na kimataifa. Aidha, masuala ya usalama wa ardhi, ufaulu wa elimu ya msingi, usimamizi wa rasilimali za umma na ulinzi wa haki za wakulima yamepewa nafasi ya pekee kama sehemu ya safari ya maendeleo ya Singida.

Tunawaalika wasomaji wetu wananchi, wadau wa maendeleo, wawekezaji na watunga sera kusoma, kutafakari na kushiriki katika kujenga Singida imara, yenye amani na fursa kwa wote. Singida ni nuru ya maendeleo, na nuru hiyo inaanzia kwa taarifa sahihi, uongozi thabiti na mshikamano wa jamii.

## MAONI YA MHARIRI

***Jarida hili ni kielelezo cha dhamira ya Mkoa wa Singida katika kusimulia maendeleo kwa uwazi, usahihi na mtazamo wa mbele. Kupitia taarifa, takwimu na simulizi za watu halisi, jarida hili linaunganisha juhudi za Serikali, wananchi na wadau wa maendeleo katika kujenga mkoa unaojitegemea, unaothamini ujuzi, na unaozingatia maendeleo endelevu. Umuhimu wa jarida hili hauishii kwenye taarifa pekee, bali ni jukwaa la kumbukumbu, uwajibikaji na msukumo wa mabadiliko chanya, likiwa chombo muhimu cha kuimarisha mawasiliano kati ya uongozi na wananchi, leo na kwa vizazi vijavyo.***

***"Tunachochea Mendeleo, Kupitia Taarifa Sahihi"***



**Glory Kimaro**
Mhariri/Chief Editor

# UONGOZI MKOA WA SINGIDA



**MHE. HALIMA DENDEGO**
MKUU WA MKOA WA SINGIDA



**DKT. FATUMA MGANGA**
KATIBU TAWALA MKOA WA SINGIDA



**MHE. GODWIN GONDWE**
MKUU WA WLAYA YA SINGIDA



**DKT. VINCENT MASHINJI**
MKUU WA WLAYA YA MANYONI



**MHE. MOSES MACHALI**
MKUU WA WLAYA YA MKALAMA



**MHE. THOMAS APSON**
MKUU WA WLAYA YA IKUNGI



**MHE. SULEMAN MWENDA**
MKUU WA WLAYA YA IRAMBA

# YALIYOMO

**Ardhi ni Dhahabu:**
Hati 800 Zakabidhiwa Iramba
Mhe. Halima Dendego



**Mifumo ya Kidijitali:**
Barcode na QR Codes
Kufungua Masoko ya Dunia




**Afya na Bima kwa Wote:**
"Mteja ni Mfalme" –
Dkt. Fatuma Mganga



**Sabasaba Skills Galla:**
Vijana wa Saba Saba
Waonesha Ujuzi wa Kujiajiri




**Ufaulu Darasa la Saba 2025:**
Singida Yapata Asilimia 81 –
Mikakati Mpya Yazinduliwa



**Amani na Uhuru:**
RC Dendego Aongoza Usafi na
Kuadhimisha Uhuru na Watoto



**Wahitimu Kutumia fursa:**
Wanaunganishwe katika
vikundi kupata mitaji.




**Kilimo na Vitendeakazi:**
"Trekta hizi zilete mavuno ya
kutosha Singida" - RC Dendego



# SALAM ZA MKUU WA MKOA WA SINGIDA



*Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, anawasalimu wananchi kwa moyo wote na kusisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya wananchi na serikali. Amesema, "Tunaposhirikiana, maendeleo ni rahisi kufanikisha," huku akihimiza mshikamano wa kijamii katika kila sekta. Katika sekta ya elimu, shule mpya za msingi na sekondari zinaendelea kujengwa, walimu wanapewa mafunzo ya kisasa ya ufundishaji, na vifaa vya kujifunzia vinapatikana ili kuongeza ubora wa elimu.*

*Katika sekta ya afya, kliniki na zahanati zinapata vifaa na mafunzo kwa wahudumu, huduma za chanjo, lishe, na afya kwa watoto na wazee zinaimarishwa, na miradi ya afya jamii inashirikisha wananchi kikamilifu. Miradi ya maji safi na usafi wa mazingira inahakikisha upatikanaji wa maji safi na vyoo vinavyofaa, huku upandaji miti na utunzaji wa mazingira ukifanywa kwa makini.*

*Kuhusu ujasiriamali wa vijana, shindano na mafunzo ya ujasiriamali yameanzishwa ili kuwapa elimu ya masoko na mbinu za kidijitali, huku mikopo na msaada wa kifedha ikitolewa kwa miradi midogo. Wananchi wanaombwa kushirikiana katika kudumisha amani na maendeleo, kuchangia mawazo na miradi ya kijamii, na kutii sheria pamoja na kushirikiana na viongozi.*

*Mhe. Dendego amepongeza vipaji na rasilimali za mkoa na kuhitimisha, "Tunaposhirikiana, hakuna kinachoweza kutuzuia kufanikisha maendeleo ya Singida."*



# "ARDHI NI DHAHABU YA MAENDELEO KWA WANANCHI" - RC DENDEGO



*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akikabidhi hati za Uiliki wa ardhi kwa baadhi ya wananchi katika kijiji cha Makunda, Wilaya ya Iramba.* | **PICHA:** GCU SINGIDA

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, aliwataka wananchi kutumia ardhi kama rasilimali ya kimkakati kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, akisisitiza umuhimu wa kuitunza na kuitumia kwa tija. Kauli hiyo ameitoa wakati wa hafla ya kukabidhi hati zaidi ya 800 za umiliki wa ardhi kwa wananchi wa Kijiji cha Makunda, Wilaya ya Iramba, ikiwa ni sehemu ya mpango wa Serikali wa kuimarisha usalama wa ardhi na kupunguza migogoro ya umiliki.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika Makunda, Mhe. Dendego amesema Serikali imeendelea kuweka mifumo ya kumuwezesha mwananchi kumiliki ardhi kihalali ili aweze kuitumia kama mtaji wa maendeleo. Ameeleza kuwa umilikishaji wa ardhi unalenga kuwawezesha wananchi kupata mikopo, kuongeza uzalishaji wa kilimo na kuimarisha ustawi wa familia, huku akisisitiza nidhamu ya matumizi sahihi ya ardhi.

"Ninawaomba wananchi, hati hizi ni heshima, ni haki na ni uchumi. Ardhi kila mwaka inaongezeka thamani; ardhi ndio dhahabu tuliyonayo mkononi. Msipate haraka ya kuuza ardhi yenu, itumieni kujijenga kiuchumi na kuboresha maisha ya familia zenu," amesema Mhe. Dendego, akionya dhidi ya matumizi yasiyo ya maendeleo yanayoweza kuleta migogoro ya kifamilia na kijamii.

Aidha, Mkuu wa Mkoa amesisitiza kuwa Serikali itaendelea kusimamia matumizi bora ya ardhi kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji, huku akihimiza wananchi kutumia hati kama dhamana ya mikopo ya maendeleo, kuwekeza katika kilimo cha mazao ya kimkakati ikiwemo alizeti, na kuhakikisha watoto wanapata elimu kwa wakati kama msingi wa maendeleo ya muda mrefu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhe. Moses Machali, aliyekuwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Iramba, amesema kukabidhiwa kwa hati hizo ni hatua muhimu katika kumuwezesha mwa-



nanchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Amewataka wananchi kuzihifadhi hati zao sehemu salama na kuzitumia kuongeza uzalishaji katika kilimo na biashara ndogondogo.

Naye Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Singida, Bi. Shamim S. Hoza, amesema Kijiji cha Makunda ni miongoni mwa vijiji 241 vilivyopo kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi katika Mkoa wa Singida. Amesema wanakijiji 899 wamenufaika na zoezi hilo, akibainisha kuwa lengo ni kupunguza migogoro ya ardhi na kuongeza thamani ya ardhi kama rasilimali ya uzalishaji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Makunda, Bw. Yesaya Daudi Seti, amesema umilikishaji wa ardhi utasaidia kuimarisha amani na mshikamano kwa kupunguza migogoro ya mipaka na kumwezesha mwananchi kuwekeza kwa uhakika. Ameishukuru Serikali kwa kuleta mpango huo na kuahidi usimamizi mzuri wa kumbukumbu za ardhi ngazi ya kijiji.

Baadhi ya wananchi waliopokea hati hizo wamesema hatua hiyo imewapa uhakika wa kisheria wa kumiliki ardhi na kuwapa fursa ya kupata mikopo ya maendeleo. Wamesema kupitia umilikishaji huo, wanatarajia kuongeza uzalishaji wa kilimo na kuboresha maisha ya familia zao.

Kwa ujumla, zoezi la kukabidhi hati za ardhi Makunda ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuhakikisha ardhi inatumika kama nyenzo ya maendeleo, kupunguza migogoro ya umiliki na kuchochea uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Iramba na Mkoa wa Singida kwa ujumla.




# ZANA ZA 'KUBOOST' KILIMO ZAMWAGWA SINGIDA




*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akikagua Powertiller 34 na kukabidhi Mikataba ya Powertiller kwa Wakurugenzi na wakuu wa Wilaya zitakazotumika kwa wakulima ndani ya Halmashauri za Mkoa wa Singida.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wote wa Mkoa wa Singida wamekabidhiwa zana za kulimia kuelekea msimu wa kilimo.

Katika maandalizi ya msimu wa kilimo, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri Mkoa wa Singida walikabidhiwa zana za kilimo na kusaini mikataba ya kimkakati inayolenga kuongeza uzalishaji wa chakula na kujaza maghala ya akiba. Hatua hii inalenga kulinda usalama wa chakula na kuongeza ustahimilivu wa uchumi wa mkoa.

Jumla ya Powertiller 34 zimegawiwa kwa wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri 5 ili kuwanufaisha wananchi wakulima Mkoa wa singida haswa katika kipindi cha maandalizi ya msimu wa kilimo. Halmashauri ya Ikungi imepata Powertiller 15, Mkalama wamepata Powetiller 12, Singida DC Powetiller 3, Iramba Powetiller na Itigi Powetiller 2.

# KIKAO KAZI CHABAINI MBIVU NA MBICHI UTENDAJI KAZI WA VIONGOZI



*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akitoa maagizo katika kikaokazi kilichofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, Desemba 2025 aliongoza vikaokazi mbalimbali vya tathmini ya utekelezaji wa majukumu kwa viongozi wa sekta mbalimbali mkoani humo, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha uwajibikaji na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kuanzia Desemba 11 hadi 13, 2025, Mkoa wa Singida uliendesha kikao kazi cha siku tatu cha tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya sekta mbalimbali. Kikao kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa kililenga kuimarisha uwajibikaji, kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi na kuweka mikakati ya kutatua changamoto. Hitimisho la kikao kiliweka dira mpya ya kuifanya Singida kung'ara zaidi kitaifa na kimataifa

Katika kikao cha Desemba 11, 2025, kila sekta iliwasilisha taarifa ya utekelezaji, changamoto zilizojitokeza pamoja na mapendekezo ya maboresho kwa kipindi kijacho. Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida alisisitiza umuhimu wa kikao hicho katika kujenga uwiano wa kimkakati, kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi, na kuhakikisha taarifa za maendeleo zinatolewa kwa wakati.

Baada ya majadiliano, wajumbe wa kikao waliahidi kutekeleza kwa vitendo maazimio yote yaliyofikiwa, hususan kuboresha usimamizi wa rasilimali, kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na kuharakisha hatua za miradi inayoendelea.

Kikao hicho kilichochukua cha siku tatu,kimetajwa kuwa hatua muhimu ya ufuatiliaji endelevu na msingi wa kuongeza tija katika maendeleo ya Mkoa wa Singida.

# KIKAO KAZI TAKWIMU ZA AFYA MKOA WA SINGIDA CHAFANA



*Katibu Tawala Msaidizi sehemu Utawala na Rasilimali watu Bw. Pancras Stephen akiendesha kikao kazi cha Afya katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Kikao kazi cha kujadili takwimu mbalimbali za afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maandalizi ya awali ya mipango ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2026/2027 katika Mkoa wa Singida kilifanyika tarehe 01 Desemba 2025 chini ya uenyekiti wa Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Bw. Pancras Stephen.

Kikao hicho kiliwakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya afya akiwemo timu ya usimamizi wa huduma za afya ya Mkoa (RHMT Singida), timu za usimamizi wa afya za Halmashauri zote (CHMT), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida (Singida RRH), Maafisa Mipango na Wahasibu wa Halmashauri, Wadau wa Afya, pamoja na baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Katika kikao hicho, washiriki walijadili kwa kina hali ya utoaji wa huduma, mwenendo wa viashiria vya afya, changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hiyo pamoja na mikakati ya maboresho kwa lengo la kuinua ustawi wa jamii. Aidha, kikao kilitoa fursa kwa wataalam na wadau kubadilishana uzoefu, taarifa na mbinu za kuimarisha mipango ya afya katika ngazi za Halmashauri na Mkoa kwa ujumla.

Kupitia Kikao kazi hicho, kimeleta manufaa makubwa kwa sekta ya afya katika Mkoa wa Singida kwa kuimarisha upatikanaji na matumizi ya takwimu sahihi katika upangaji wa mipango na utekelezaji wa shughuli za afya.

Kupitia majadiliano ya pamoja, wadau wamepata fursa ya kubaini changamoto zinazoathiri utoaji wa huduma na kuweka mikakati thabiti ya kuzitatua kwa wakati. Vilevile,

kikao kimeongeza ushirikiano kati ya RHMT, CHMT, Halmashauri na wadau mbalimbali wa afya, jambo linalowezesha kuratibu rasilimali na juhudi za pamoja kwa ufanisi zaidi.

Pia kiliweka msingi imara wa maandalizi ya mipango ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa kuzingatia tathmini ya mwaka uliopita, mahitaji ya sasa ya jamii na vipaumbele vya sekta ya afya, hivyo kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.







## BIMA YA AFYA KWA WOTE



# "WATOTO WASHIBE KABLA YA KUPEWA DAWA ZA KINGA TIBA" - RC DENDEGO



*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akizungumza na Wahudumu wa Afya katika kikaokazi kuhusu Chanjo ya Kichocho na Minyoo kwa watoto wadogo Ml Mkoa wa Singida .* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, ameagiza Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha watoto wote wanakula vizuri kabla ya kupewa dawa za kinga tiba dhidi ya kichocho na minyoo, akisisitiza kuwa hatua hiyo ni muhimu kwa usalama na ufanisi wa matibabu. Akizungumza katika kikao cha kuweka mpango mkakati wa utoaji wa kinga tiba kwa watoto wenye umri wa miaka 5 hadi 14, kilichofanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mhe. Dendego alisema watoto wasipewe dawa wakiwa na njaa kwani inaweza kuleta athari za kiafya na kupunguza ufanisi wa kampeni hiyo.

Aidha, aliwataka viongozi wa halmashauri kutathmini utekelezaji wa mpango huo kwa umakini, hususan kwa kuwatambua na kuwafikia watoto wa mitaani ambao mara nyingi hukosa lishe ya uhakika na wanaweza kuachwa nyuma katika zoezi hilo. Mhe. Dendego amesisitiza kuwa jukumu la kuhakikisha watoto wanalindwa na wanapata huduma hii muhimu bila hatari yoyote ni la halmashauri zote mkoani Singida.









*"Watoto wa Shule wapewe Chakula kabla ya kupata chanjo za Kichocho na Minyoo ili kuepusha madhila kwa watoto wetu ambao ni tegemeo la kizazi cha taifa hili kwa baadae."*

**Mhe. Halima Dendego,** Mkuu wa Mkoa wa Singida





# "MTEJA NI MFALME" – DKT. FATUMA MGANGA



*Katibu Tawala Mkoa wa Singida Dkt. Fatuma Mganga, katika kikao kazi kujadili tathmini ya Bima ya Afya kwa Wote Mkoa wa Singida.* | ***PICHA:*** GCU SINGIDA

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Mganga, awataka wahudumu wa afya mkoani Singida kuzingatia maadili, utu na kuwajali wananchi wanapotoa huduma za afya, akisisitiza kuwa mteja ndiye mhimili mkuu wa mafanikio ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote. Ameyasema hayo wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote kilichofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA) mkoani Singida.

Akizungumza katika kikao hicho kilichowakutanisha waganga wafawidhi wa vituo vya afya mkoa wa Singida, Dkt. Mganga amesema Serikali inaanza utekelezaji wa bima hiyo kwa majaribio kwa makundi maalum, hivyo ni muhimu wahudumu wa afya kuwahudumia wananchi kwa weledi ili kila mmoja anufaike na mpango huo. Amesema huduma duni au lugha isiyofaa inaweza kuwakatisha tamaa wananchi na kudhoofisha lengo la Serikali la kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa wote.

Dkt. Mganga amewataka pia wasimamizi wa huduma za afya kufanya marekebisho na kuboresha utoaji wa huduma katika vituo vya afya ili wananchi wasijutie kujiunga na mfuko wa bima ya afya, hususan kwa makundi maalaum ambayo Serikali itayalipia gharama. Amesisitiza kuwa mazingira ya vituo vya afya yanapaswa kuboreshwa ili mwananchi anapofika ajisikie kuthaminiwa na kupata huduma stahiki.

Aidha, amezitaka taasisi za afya kuhakikisha zinalipa madeni yanayodaiwa na Bohari ya Dawa (MSD) kwa wakati, ili kuwezesha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na huduma muhimu zinazokidhi mahitaji ya wananchi. Amesema upatikanaji wa dawa na vifaa ni msingi wa utoaji huduma bora na mafanikio ya bima ya afya kwa wote.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida amewataka wahudumu wa afya kuvaa mavazi rasmi yanayotambulika ili kuongeza uaminifu kwa wagonjwa na kuimarisha taswira ya sekta ya afya. Ameongeza kuwa matumizi ya lugha nzuri na yenye staha kwa wagonjwa ni msingi muhimu wa kudumisha uhusiano mzuri kati ya wahudumu wa afya na wananchi.

Kwa niaba ya waganga wafawidhi wote wa mkoa wa Singida, viongozi wa vituo vya afya wameahidi kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Katibu Tawala wa Mkoa kwa kuboresha huduma za afya, kuongeza uwajibikaji na kuhakikisha vituo vinaingiza mapato yatakayosaidia kuendeleza huduma. Wamesema dhamira yao ni kuufanya Mkoa wa Singida kuwa mfano wa utoaji huduma bora za afya nchini Tanzania.

Kikao kazi hicho pia kimewakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya afya, wakiwemo wawakilishi wa NHIF, TIRA, MSD na taasisi nyingine, ambao waliwasilisha mada na maelezo kuhusu mwelekeo wa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, hatua inayotarajiwa kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma za afya kwa wananchi wote.







# "TUMIENI VIZURI TEKNOLOJIA KUENDANA NA ELIMU YENU" RC DENDEGO






*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akitkabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu katika Chuo cha Uhasibu TIA Singida.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego, ameshiriki katika Mahafali ya 23 ya Chuo cha Uhasibu (TIA)Kampasi ya Singida kama mgeni rasmi.

Katika hotuba yake Mhe. Dendego amewasisitiza vijana kutumia vizuri mitandao ya kijamii kuendana na mabadiliko ya teknolojia ili kunufaika na mitandao hiyo katika kujumuika na wengine(Networking), kukuza biashara na kujifunza mambo mapya.

Kadhalika amewahimiza kuwa waaminifu na wanyenyekevu,wabunifu na waadilifu kwa kutochoka kujifunza mambo mapya kila siku.

Jumla ya wanafunzi 1,490 wamehitimu elimu ya Astashahada, Stashahada na Shahada.

# TUJIKITE KUWAFUNDISHA VIJANA WETU MAADILI – RC DENDEGO



Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akitkabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu katika Chuo cha Ufundi na Marekebisho kwa watu wenye Ulemavu (Saba Saba) Mkoa wa Singida. | **PICHA:** GCU SINGIDA

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, awaasa vijana wahitimu wa Chuo cha Ufundi na Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu (Saba Saba) kujitunza na kufuata maadili watakaporejea mitaani baada ya kumaliza masomo yao, akisisitiza kuwa ujana ni rasilimali isiyorudi na ukiupoteza huathiri maisha ya baadaye.

Akizungumza wakati wa mahafali ya chuo hicho, Mhe. Dendego aliwataka vijana kuepuka matumizi ya dawa za kulevya na ngono zembe, akiwakumbusha msemo wa "Kula nanasi kwataka nafasi", akimaanisha umuhimu wa kusubiri muda muafaka kabla ya kuingia katika mahusiano ili kuepuka mimba za utotoni na magonjwa ya zinaa.

Aidha, aliwaelekeza wakurugenzi, maafisa ustawi na maendeleo ya jamii kuhakikisha vijana wanaunganishwa katika vikundi na kupewa mitaji ili kuwawezesha kuanzisha shughuli za uzalishaji mali badala ya kubaki mitaani bila ajira. Alitoa wito kwa waajiri kuacha kuwaona vijana kama dhaifu, badala yake wawapatie ushirikiano na fursa za kazi.

Mhe. Dendego pia aliwasisitiza vijana kuepuka uharibifu wa rasilimali za taifa kama njia ya kutafuta suluhu ya changamoto zao, bali kuzitumia kwa manufaa yao. Aliwahimiza wahitimu kuwasilisha mawazo ya miradi yao ili kupata mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri kwa makundi maalumu, hatua itakayowawezesha kuanzisha biashara na kukuza uchumi wao.

Kwa upande wake, Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Singida, Bi. Yasinta Alute, aliyemwakilisha Mganga Mkuu wa Mkoa, alisema kupungua kwa changamoto za afya ya akili miongoni mwa vijana kunatarajiwa kutokana na kuongezeka kwa uelewa na elimu pamoja na fursa za ajira zitokanazo na ujuzi wanaoupata vyuoni. Alisema kipato kitakachotokana na ujuzi huo kitawasaidia vijana kupata utulivu wa fikra na kupunguza msongo wa mawazo.

Akizungumza kwa niaba ya Afisa Elimu wa Mkoa, Bi. Sarah Mkumbo ambaye ni Afiaa elimu ya watu wazima,aliwahakikishia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kuwa serikali inaendelea kuboresha mazingira rafiki ya kujifunzia, ikiwemo miundombinu wezeshi ili kuwarahisishia elimu. Aliwaomba kuwa mabalozi kwa vijana wengine wenye ulemavu ili wajitokeze kujiunga na mafunzo ya ufundi.

Naye Mkuu wa Chuo hicho, Bi. Fatuma Malenga, alisema chuo kimepata mafanikio makubwa kupitia programu ya wanagenzi ambayo imeongeza mwamko kwa vijana kujifunza fani za ufundi. Hata hivyo alitaja changamoto zinazokikabili chuo hicho kuwa ni pamoja na kuibiwa kwa uzio wa chuo, ukosefu wa ukumbi wa mihadhara na baadhi ya wanafunzi kushindwa kuhudumiwa ipasavyo kutokana na hali duni ya wazazi wao..





# MAADILI NA ELIMU KUWA KIPAUMBELE KWA WANAFUNZI MKOA WA SINGIDA



*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akihutubia katika kakao na Wakuu wa Shule Mkoa wa Singida Kilichofanyka katika Manispaa ya Singida.* | **PICHA:** GCU SINGIDA

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, ametoa wito kwa Walimu wa Mkoa wa Singida kujikita kikamilifu katika kuimarisha maadili na mwenendo wa vijana, akisisitiza kuwa msingi wa tabia njema ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa.

Ameyasema hayo akifungua kikao kazi cha Waalimu Wakuu wa Shule za Msingi Desemba 10,2025 kilichojadili na kufanya tathmini kilichofanyika katika Manispaa ya Singida, Mhe. Dendego amebainisha kuwa malezi ya vijana ni jukumu shirikishi linalohitaji usimamizi makini, hekima na mwongozo wa walimu ili kuhakikisha Singida inaendelea kulea kizazi chenye nidhamu, uwajibikaji na uzalendo.

Katika hotuba yake, Mhe. Dendego aliwapongeza Walimu Wakuu wa Mkoa wa Singida kwa kazi kubwa wanayoifanya ambayo imeendelea kuuweka mkoa katika nafasi nzuri kitaaluma. Amezielekeza pia Halmashauri zote kuongeza nguvu, usimamizi na rasilimali katika sekta ya elimu, akisisitiza kuwa mafanikio yanayotarajiwa mwaka ujao yatategemea uimara wa mipango, ubunifu na mshikamano kati ya walimu na viongozi wa elimu.

Ripoti iliyosomwa na Ofisi ya Elimu Mkoa wa Singida imeonesha kuwa mkoa umeendelea kufanya vizuri katika matokeo ya shule za msingi kwa mwaka 2025, ambapo kiwango cha ufaulu kimefikia zaidi ya asilimia 80. Takwimu hizi zimeelezwa kuwa ni ishara ya maendeleo chanya ukilinganisha na miaka iliyopita, na uthibitisho wa kazi madhubuti ya walimu, usimamizi wa viongozi wa elimu na jitihada za Serikali ya mkoa katika kuinua kiwango cha elimu.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Afisa Elimu wa Mkoa wa Singida, Mwl. Makwasa Bulenga, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhe. Godwin Gondwe, pamoja na wadau mbalimbali wa elimu walioungana kujadili mikakati ya kuimarisha maadili na taaluma. Ushiriki wao umeonyesha dhamira ya pamoja ya kuendelea kuboresha sekta ya elimu na kuhakikisha Mkoa wa Singida unaendelea kuwa mfano wa mafanikio kitaaluma na kimaadili nchini.



# MUAROBAINI UFAULU SHULE YA MSINGI WAPATIKANA, RAS SINGIDA ATOA MIKAKATI.



*Katibu Tawala Mkoa wa Singida Dkt. Fatuma Mganga akiwa na Wanafunzi katika SHule ya Msingi Sophia wakati wa Ziara ya kukagua Miradi ya Elimu Mkoa wa Singida.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Daktari Fatuma Mganga ametoa wito kwa walimu wa shule za msingi kuongeza ubunifu katika ufundishaji ili kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba.

Akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Shule ya Msingi Sophia, alisema mbinu madhubuti za ufundishaji ndizo zitakazowezesha wanafunzi kuwa na uelewa mpana na maandalizi bora ya mitihani yao. Ameeleza kuwa walimu wanapaswa kuwahimiza wanafunzi kufanya mazoezi mengi ya masomo, jambo litakaloongezea uwezo na kuondoa hofu ya mitihani.

Akiendelea kuzungumza, Katibu Tawala Dkt.Mganga amesisitiza umuhimu wa walimu kuhakikisha wanafunzi wanakuwa nadhifu na wenye usafi muda wote. Amesema suala la usafi ni sehemu ya malezi na maandalizi ya mwanafunzi kujiandaa na hatua inayofuata ya elimu. Kadhalika, amewataka wanafunzi kuheshimu muda wa kufika shuleni na kuwatii walimu wao, sambamba na kuhakikisha mazingira ya shule na madarasa yanabaki kuwa safi ili kuweka msingi wa nidhamu na utendaji bora.

Afisa Elimu wa Mkoa wa Singida akapata nafasi ya kuzungumza na wanafunzi hao na kuwataka kuongeza bidii katika masomo yao. Ameahidi kuanzisha mbinu shirikishi na rafiki kwa walimu ambazo zinalenga kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa darasa la saba kuanzia mwaka ujao. Aidha, amesema kuwa mitihani ya mazoezi ya kila mwezi itaanza kutolewa kuanzia Januari, na wanafunzi watakaofanya vizuri watazawadiwa ili kuongeza ari ya kujifunza na ushindani chanya miongoni mwao.

Kwa upande wa wanafunzi, Lucas Mwagoko ameonesha kujawa na hamasa na kuahidi kusoma kwa bidii ili kufaulu kwa kiwango cha juu katika mtihani wao wa taifa wa darasa la saba mwaka 2026. Amesema hotuba na maagizo yaliyotolewa yamewapa motisha ya kufanya kazi kwa bidii na kujiandaa mapema.

Ziara hiyo pia ilihusisha ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayoendelezwa na Serikali Kuu katika Shule ya Msingi Sophia, ikiwemo ujenzi wa madarasa matatu, nyumba ya mwalimu na matundu 38 ya vyoo. Utekelezaji wa miradi hiyo unaelezwa kuwa sehemu ya mpango wa Serikali kuboresha miundombinu ya elimu na kuweka mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji.

Katika matokeo ya darasa la saba kitaifa mwaka 2025 Mkoa wa Singida umepata wastani wa 81.

Kupitia maboresho hayo, Serikali inaendelea kuwaandaa wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa kuwajengea mazingira salama na rafiki ya kujifunzia. Hii inajumuisha ujenzi wa madarasa mapya, mabweni na maktaba, upatikanaji wa vitabu vya kutosha, vifaa vya maabara, TEHAMA, na kuongeza nguvu kazi ya walimu. Hatua hizo zinahakikisha kuwa wanafunzi wanapofika sekondari wanakutana na mazingira yaliyoboreshwa yanayowawezesha kusoma kwa ufanisi na kufikia malengo yao ya kitaaluma.

.





# MIFUMO YA KIDIGITALI KUWAFUNGULIA MILANGO WAJASIRIAMALI




*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, katika picha ya pamoja na Wajasiliamali na wakufunzi wa Msimbomlia (Barcodes/QR Codes) waliopata elimu juu ya Matmizi ya Msimbomlia katika bidhaa za Wajasiliamali Mkoa wa SIngida.* | ***PICHA:*** GCU SINGIDA

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, alizindua mafunzo ya kujenga uwezo kwa wajasiriamali kuhusu matumizi ya GS1 Barcodes na QR Codes, akisisitiza kuwa mifumo hiyo ya kidijitali ndiyo njia ya kuwafungulia wajasiriamali milango ya masoko ya kitaifa na kimataifa. Mafunzo hayo yalifanyika chini ya kauli mbiu "GS1 Barcodes: Kiungo chako kwa wauzaji rasmi", yakilenga kuwajengea wajasiriamali uelewa wa mifumo ya utambulisho wa bidhaa inayotambulika duniani kote.

Semina hiyo iliwezeshwa na GS1 Tanzania kwa ushirikiano na taasisi mbalimbali za serikali ikiwemo TRA, BRELA na wadau wengine, ambao wameeleza kwa kina namna wajasiriamali wanaweza kupata barcode na QR code kisheria, hatua zinazowaepusha na ulaghai na kuwalinda dhidi ya matumizi mabaya ya bidhaa zao na makampuni mengine. Aidha, hatua hii ya kidijitali inatarajiwa kuongeza thamani ya bidhaa za Singida na kuziwezesha kupenya kwenye masoko makubwa duniani.

Akizungumza wakati wa ufunguzi, Mhe. Dendego amewataka wajasiriamali wa Singida kuchangamkia fursa hii ya kimkakati, akibainisha kuwa Mkoa wa Singida una bidhaa nyingi zenye ubora wa juu lakini bado hazijapata nafasi ya kutamba kimataifa kutokana na kukosa utambulisho wa kidijitali. "Kundi hili la wajasiriamali ni injini ya uchumi wa Singida. Sisi tuna bidhaa nzuri sana, lakini bila mifumo ya kimataifa kama barcode hatutaifika dunia. Soko la kimataifa linaendeshwa kidijitali, na kama hatuko huko, basi hatutapenya," amesema.

Aliongeza kuwa Singida ni kitovu cha nchi na hivyo ni mahali sahihi kufunguliwa kwa ofisi ya pili ya GS1 Tanzania. "Ikiwa mtapanga kufungua ofisi mpya nchini, basi Singida ndiyo mahali pake. Tupo katikati ya Tanzania, wajasiriamali watapata huduma kwa urahisi, na hilo litakuwa chachu ya maendeleo makubwa," amesema.

Mkuu wa Mkoa pia alisisitiza umuhimu wa kulinda amani ili biashara ziendelee kustawi. "Amani ikitoweka, biashara hazipo. Tunaishukuru serikali kwa kutengeneza mazingira bora ya biashara huru. Basi nasi tuitumie fursa hii kutangaza Singida duniani," amesisitiza.



Kwa upande wake, Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Rasilimali Watu, Bw. Pancras Stephen, amesema mafunzo hayo yamekuja wakati sahihi, hasa kutokana na ukweli kwamba hata watumishi wa umma wengi wanajihusisha na ujasiriamali. Amesema, "Ujasiriamali wa sasa uko kwenye mifumo ya kidijitali. Tunawaomba mjenge uthubutu na kutumia maarifa haya kupiga hatua katika familia, jamii na taifa."

Aidha Katibu Tawala Msaidizi – Biashara na Uwekezaji, Bi. Donatira Vedasto, amewataka wajasiriamali kuwa mabalozi wa Singida kupitia bidhaa zao. "Baada ya mafunzo, kila mmoja achukue hatua. Singida inazalisha bidhaa bora sana, lakini bila barcode hatuwezi kufika soko la kimataifa," amesema.

GS1 Tanzania, kupitia wakufunzi wake, wameahidi kuendelea kutoa mafunzo katika wilaya zote za Singida. Wamesema wajasiriamali wengi wamekuwa wakikosa nafasi ya kuuza kimataifa kwa sababu hawana elimu ya barcode. "Mafunzo haya yatafanya kila mjasiriamali awe na hamu ya kufika soko la kimataifa. Tutafika kila halmashauri kuhakikisha hakuna anayebaki nyuma,".

Nao Wajasiriamali walioshiriki semina hiyo walitoa shuhuda mbalimabli wakisema matumizi ya barcode yamewasaidia kuaminika katika supermarkets na malls, hatua iliyoimarisha mauzo na kuwapa nafasi ya kutambulika rasmi na serikali. Wameshukuru serikali kwa kuweka miundombinu ya kidijitali na kuwawezesha kufikia masoko makubwa nje ya nchi.

Hatua hii ya kidijitali imeelezwa kuwa mwanzo wa mageuzi makubwa ya biashara Singida, huku serikali na wadau wakiahidi kuendelea kuweka mazingira rafiki kwa ukuaji wa uchumi wa wajasiriamali.









# RC DENDEGO ATATUA MGOGORO WA ARDHI



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, 3 Desemba 2025 alimkabidhi rasmi Hati ya Umiliki Bi. Mwasiti Abdallah Marambi kwa kiwanja kilichokuwa na mgogoro kilichopo eneo la Unyankhae, Manispaa ya Singida. Tukio hilo lilihitimisha mgogoro wa ardhi kati ya Bi. Mwasiti na Bw. James Michael Mmasy, baada ya mchakato wa usuluhishi uliofanywa na Mhe. Dendego.

Katika kuendeleza misingi ya uwajibikaji na uongozi wa vitendo, Mhe. Halima Dendego ameonyesha dhamira thabiti ya kuifanya Singida iendelee kusimama kwenye haki, utulivu na maendeleo. Utatuzi huu ni sehemu ya juhudi zake endelevu za kuimarisha usimamizi wa ardhi na kuhakikisha kila changamoto inapata suluhu ya kudumu kwa manufaa ya ustawi wa mkoa.

Hatua hii inaendeleza taswira ya mkoa kuelekea Jiji la Singida unaoongozwa kwa uadilifu, nidhamu na maamuzi yenye tija.





# DENDEGO AWAPA WATOTO TABASAMU UHURU DAY




*Mkuu wa Mkoa wa Singida katika Picha ya pamoja na Watoto wenye mahitaji maalum kusherehekea Siku yake ya Kuzaliwa.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego ameungana na watoto wa Kituo cha Malaika wa Matumaini kilichopo Ititi, Manispaa ya Singida, katika kusherehekea maadhimisho ya miaka 64 ya Uhuru wa Tanganyika.

Katika siku hiyo ambayo pia inaendana na kumbukizi ya siku yake ya kuzaliwa, Mkuu wa Mkoa alitumia muda huo kufurahi na watoto hao wenye mahitaji mbalimbali pamoja na kuwapa hamasa.

Aidha, alitumia hafla hiyo kuwasisitiza wakazi wa Singida kuendeleza amani iliyopo mkoani humo, kufanya shughuli zao za kila siku kwa utulivu na kuwa na uhakika wa usalama wao

# RC DENDEGO AONGOZA ZOEZI LA USAFI MKOA WA SINGIDA



MMkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, aliongoza zoezi kubwa la usafi mkoani Singida ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Maadhimisho ya Uhuru wa Tanzania. Akizungumza na wananchi, RC Dendego aliwasisitiza kuendeleza desturi za kuvumiliana, kusikilizana kwa ustaarabu, na kutatua changamoto kwa utulivu na hekima. Alisema mkoa una mifumo rasmi ya utoaji wa huduma kupitia ngazi za mtaa hadi mkoa, hivyo wananchi wanayo nafasi ya kusikilizwa na kutatuliwa changamoto zao. "Amani yetu ndiyo maendeleo yetu, ndiyo uhuru wetu, na ndiyo uchumi wetu Singida," amesisitiza.

Alisema kuwa usafi ni jukumu la kila mmoja na ni sehemu muhimu ya kulinda afya na mazingira, akihimiza zoezi hilo liwe endelevu badala ya kuwa la siku moja. RC Dendego pia amewaasa vijana kuendelea kulinda amani ya nchi na kurithi tunu za amani zilizoachwa na waasisi wa taifa. Ameeleza kuwa amani ndiyo msingi wa maendeleo, na hivyo vijana na wananchi kwa ujumla wanapaswa kuepuka vikundi vyenye kuchochea vurugu au uvunjifu wa utulivu.

Katika hotuba yake, RC Dendego aliwapongeza watumishi wa umma, wananchi na vijana waliojitokeza kushiriki

zoezi hilo, akisema wameonyesha uzalendo wa hali ya juu. Ametahadharisha dhidi ya kudanganywa na watu wanaochochea migogoro au uharibifu wa mali za jamii kwa kisingizio cha kutatua matatizo. "Hakuna maendeleo yanayotokana na kuchoma miundombinu, kufanya vurugu au kupigana; badala yake tunarudi nyuma," amesema. Aidha, amewataka wananchi kuwasilisha changamoto kwa viongozi wao kwa utulivu kwani wote "wanapatikana na wako tayari kusikiliza."

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mhe. Moses Machali, alipongeza juhudi za Mkoa wa Singida katika kuimarisha amani, akiwataka wananchi kuwa mabalozi wa utulivu. Amehimiza wananchi kutafakari mifano ya mataifa yaliyoharibikiwa kutokana na vurugu, akisema Tanzania inapaswa kuendelea kuthamini amani iliyojengwa na wazee wa nchi. Ameitaka jamii kutumia maadhimisho ya miaka 64 ya Uhuru wa Tanganyika kama fursa ya kuenzi umoja na ushirikiano kama njia bora ya kutatua changamoto.





# MKOA WA SINGIDA WAENDELEA KUFUATILIA MADENI YA WAKULIMA WA TUMBAKU - WAWILI WASHIKILIWA



Mkoa wa Singida unaendelea kuchukua hatua madhubuti kufuatilia malipo ya madeni ya wakulima wa tumbaku kwa msimu wa kilimo 2024/2025, kufuatia ucheleweshaji wa malipo kwa zaidi ya miezi minne unaohusisha makampuni matatu ya ununuzi wa tumbaku.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, Katibu Tawala Msaidizi wa Huduma za Uzalishaji na Uchumi Mkoa wa Singida, Bw. Stenslaus Beatus Choaj, alisema ucheleweshaji huo ni ukiukwaji wa mikataba kati ya vyama vya wakulima na makampuni husika.

Alisema Mkoa umeanza kuwashikilia wawakilishi wa makampuni mawili ya Biexen Company Ltd na Magefa Growers Ltd kwa kushindwa kutoa maelezo ya kuridhisha mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, huku kampuni ya Famous Rock Private Ltd ikikaidi kabisa wito wa kufika au kutuma mwakilishi wake katika vikao vilivyoitishwa.

Hatua hizi zimelenga kulinda haki za wakulima na kuhakikisha wanalipwa fedha zao kwa mujibu wa makubaliano.

Kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Tumbaku Tanzania, katika msimu wa kilimo 2024/2025 jumla ya kilo 1,742,651.33 za tumbaku zimenunuliwa mkoani Singida zenye thamani ya Dola za Marekani 4,188,969.81. Kati ya fedha hizo, Dola 3,384,158.78 sawa na asilimia 80.79 zimeshalipwa, huku Dola 804,811.03 sawa na asilimia 19.11 bado ni madeni. Madeni hayo yanadaiwa na Magefa Growers Ltd (USD 465,211.19), Biexen Company Ltd (USD 297,355.18) na Famous Rock Private Ltd (USD 42,344.66).

Bw. Choaj amewahakikishia wakulima kuwa Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inaendelea kuchukua hatua za haraka ikiwemo kusimamia mauzo ya tumbaku za makampuni husika ili fedha zipatikane kwa ajili ya kuwalipa wakulima.

Amesisitiza kuwa Mkoa wa Singida hautavumilia kampuni yoyote inayokiuka mikataba na kuchelewesha malipo ya wakulima, akizitaka kampuni zote za ununuzi wa mazao ya kilimo kuwa waaminifu na kuwaheshimu wakulima.

# EXIT MEETING: SINGIDA KUWEKA MIKAKATI YA UKAGUZI WA NDANI KUPUNGUZA HOJA KATIKA MKOA WA SINGIDA



Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dkt.Fatuma Mganga ameongoza kikao cha tathmini ya kufunga hoja za ukaguzi Desemba 23,2025, ikiwa ni mkutano unaofanyika mwishoni mwa zoezi la ukaguzi ambapo wakaguzi hukutana na uongozi wa taasisi iliyokaguliwa.

Exit meeting ya wakaguzi ina dhumuni la kufunga rasmi zoezi la ukaguzi kwa kuwakutanisha wakaguzi na uongozi wa taasisi iliyokaguliwa ili kuwasilisha na kujadili matokeo ya awali ya ukaguzi.

Katika mkutano huu, wakaguzi walieleza hoja kuu walizobaini ikiwemo dosari, udhaifu katika mifumo au taratibu, pamoja na mambo mazuri yaliyopo, huku wakihakikisha kuwa kuna uelewa wa pamoja juu ya hoja hizo na kutoa nafasi kwa menejimenti kuuliza maswali, kutoa ufafanuzi au maelezo ya ziada pale inapobidi.

Kadhalika,wajumbe walijadili mapendekezo ya wakaguzi kwa lengo la kuboresha utendaji na udhibiti wa ndani, kupokea majibu ya awali ya menejimenti kuhusu hatua wanazokusudia kuchukua, na kueleza hatua zinazofuata kama vile muda wa kuwasilisha ripoti ya mwisho na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dkt. Mganga alisema kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Singida itaendelea kuimarisha uwajibikaji, uwazi na ushirikiano kati ya wakaguzi na taasisi iliyokaguliwa.

Kadhalika alitoa pongezi kwa Wajumbe wa Menejimenti waliofanikiwa kuondoa hoja mbalimbali na kuwaelekeza kuendelea kufuata kanuni na taratibu za utendajikazi sambamba na matumizi ya mifumo kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji katika Utumishi wa Umma.

# HALMASHAURI ZATAKIWA KUKAMILISHA MIKOPO YA ASILIMIA 10 KABLA YA DESEMBA 15




*Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dkt. Fatuma Mganga akizungumza na Wakurugenzi, Maafisa Maendeleo na Makatibu Tawala wa Halmashauri za Mkoa wa Singida juu ya khakikisha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu wanapata Mkikopo ya 10% ambazo Serikali imeelekeza.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Mganga, amezitaka halmashauri zote za mkoa huo kuhakikisha zinakamilisha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ifikapo Desemba 15, 2025. Agizo hilo lililelenga kuimarisha upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa makundi maalum na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Dkt. Mganga alitoa maelekezo hayo jana wakati wa kikao kazi cha Kamati za Uratibu na Uhakiki wa Mikopo ya Asilimia 10 ngazi ya mkoa na wilaya, kilichowakutanisha Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, Waratibu wa Madawati ya Huduma Ndogo za Kifedha pamoja na Waratibu wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) kutoka halmashauri zote za Mkoa wa Singida.

Akisisitiza umuhimu wa kuzingatia muda na taratibu, Dkt. Mganga aliagiza maombi yote ya mikopo yaliyopo kwenye mchakato—kuanzia ngazi ya vikundi, Divisheni ya Maendeleo ya Jamii hadi ofisi za Wakurugenzi—yahitimishwe kwa wakati. Alisema ucheleweshaji unaathiri walengwa na kudhoofisha dhamira ya serikali ya kuwezesha maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi.

Aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipanga kuhakikisha wananchi wanapata fursa za kiuchumi kwa uwazi na ufanisi, huku utoaji wa mikopo ya asilimia 10 ukiwa miongoni mwa mikakati muhimu. Kwa Mkoa wa Singida, alisema ni wajibu wa wadau wote kuhakikisha taratibu za utoaji na urejeshaji wa mikopo zinafuatwa kikamilifu ili kuongeza mzunguko wa fedha na kunufaisha walengwa wengi zaidi.

Kwa upande wa TASAF, Dkt. Mganga alisema mpango huo





umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya kaya maskini. Alieleza kuwa kupitia TASAF, kaya hupokea ruzuku za fedha taslimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji muhimu kama afya na elimu, sambamba na kuwezeshwa kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa kwa lengo la kujenga uendelevu wa kiuchumi.

Alifafanua kuwa jumla ya vikundi 70 vya kuweka na kukopa vilivyoundwa chini ya uratibu wa TASAF vina kiasi cha Shilingi milioni 662.629 kinachoendelea kuzunguka katika vikundi hivyo. Aidha, aliwataka Maafisa Maendeleo ya Jamii kuendelea kuwahamasisha walengwa wa TASAF kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali ili hatimaye waweze kujitegemea na kujiondoa kwenye orodha ya wanufaika wa mpango huo.

Awali, Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Mikopo ya Asilimia 10, Bi. Donatila Vedasto, alisema kikao hicho kililenga kufanya tathmini ya utoaji wa mikopo katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2025/2026 kuanzia Julai hadi Septemba, ili kubaini changamoto zilizojitokeza na kuchukua hatua stahiki.

Bi. Donatila alisema katika kipindi hicho, halmashauri nne za Mkoa wa Singida zimefanikiwa kutoa mikopo ya asilimia 10 yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.078 kwa vikundi 86. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 797.835 ni mapato ya ndani ya halmashauri huku Shilingi milioni 280.280 zikiwa ni fedha za marejesho, hatua aliyosema inaonesha kuimarika kwa mzunguko na uendelevu wa mfuko huo.

Kwa ujumla, kikao kazi hicho kimeweka msisitizo mpya wa utekelezaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wakati, uwazi na uwajibikaji, sambamba na kuimarisha uratibu kati ya sekta ya maendeleo ya jamii na mipango ya kunusuru kaya maskini. Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza fursa za kiuchumi, kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo jumuishi kwa wananchi wa Mkoa wa Singida.







# "UONGOZI NI DHAMANA, TUWATUMIKIE VYEMA WANANCHI" DKT. FATUMA MGANGA



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dkt. Fatuma Mganga akizungumza na Waheshimiwa Madiwani katika Ukumbi wa Ofisi ya Manispaa ya Singida wakati wa Uapisho wa Madiwani hao.* | ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Mganga, aamesema kuwa uongozi ni dhamana na uwajibikaji hivyo Waheshimiwa Madiwani wapya wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida waende kulizingatia hilo .

Hayo aliyasema wakati wa Uapisho wa Madiwani wakati akihutubia Baraza la Kwanza jipya la Halmashauri ya Singida ambalo Madiwani hao waliapishwa na kuanza rasmi majukumu ambayo yatadumu kwa miaka mitano.






# ZIARA NA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO MKOA WA SINGIDA



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dkt. Fatuma Mganga akifanya ukaguzi wa Miundombinu ya Elimu katika zaira maalum ndani ya Halmashauri ya Mkalama.*
| ***PICHA:*** *GCU SINGIDA*

Ziara ya Katibu Tawala Mkoa wa Singida ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo wilayani Mkalama, Desemba 16, 2025.











# RC DENDEGO KUPOKEA PONGEZI KWA UTENDA KAZI KUIINUA SINGIDA








Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, 1 Desemba 2025 alipokea tuzo ya Pongezi kutoka kwa taasisi ya PPD iliyopo mkoani Singida.

Dhumuni la tuzo hiyo ilikuwa ni kuutambua mchango wake wa dhati katika kudumisha amani wakati wote kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu katika Mkoa wa Singida.

Katika hafla hiyo Mhe.Dendego aliwaasa vijana kuendelea kuitunza amani tuliyonayo hapa nchini kwa kutumia majukwaa yao vizuri katika kuilinda amani iliyopo.

Naye Mkurugenzi wa PPD, Bw. Maulid Mrisho akizungumza kwa niaba ya wajumbe wa Taasisi hiyo aliahidi kushirikiana moja kwa moja katika kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Serikali ili kuhakikisha vijana wanan-ufaika katika kupata maendeleo, sambamba na watu wenye mahitaji maalum(walemavu).

# SINGIDA DC'S TEACHERS CONNECT YAFANA









Matukio katika picha ya yaliyojiri tarehe 29, Novemba 2025 katika hafla iliyowakutanisha Waalimu wote kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa lengo la kufurahia mambo mbalimbali waliyofanikiwa kuyafanikisha katika wajibu wao kama waalimu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mh e.Halima Dendego akiwa Mgeni Rasmi wa Shughuli hiyo aliwatia moyo waalimu kuendelea kujituma zaidi na kuwaahidi kuwa Serikali imejipanga vizuri kuendelea kuwaandalia mazingira bora na rafiki ya wao kuendelea kufundisha wanafunzi kwa matokeo bora zaidi.

Kadhalika Katika hafla hiyo zawadi na tuzo mbalimbali mbalimbali zilitolewa kwa waalimu.

# HABARI PICHA YA MATUKIO MBALIMBALI



## SALAM ZA KRIMAS NA MWAKA MPYA

OFISI YA MKUU WA MKOA
WA SINGIDA



OFISI YA MKUU WA MKOA
WA SINGIDA

# Heri ya Krismasi



**MHE. HALIMA DENDEGO**
MKUU WA MKOA WA SINGIDA

**Mhe. Halima Dndego,**
Mkuu wa Mkoa wa Singida,
Anaungana na Mheshimiwa
**Dkt. Samia Suluhu Hassan,**
Rais wa Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania Kuwatakia
Heri ya Sikukuu ya Krismas
Wana Singida na Watanzania
kwa Ujumla.

Tusherehekee Sikukuu hii kwa
Amani, Upendo na Utulivu
tukidumisha Mshikamano
wa Kitaifa.

# Heri ya Krismasi



**DKT. FATUMA MGANGA**
KATIBU TAWALA MKOA WA SINGIDA

**Dkt. Fatuma Mganga;**
Katibu Tawala Mkoa wa Singida,
Anaungana na Mheshimiwa
**Dkt. Samia Suluhu Hassan,**
Rais wa Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania Kuwatakia
Heri ya Sikukuu ya Krismas
Wana Singida na Watanzania
kwa Ujumla.

Tusherehekee Sikukuu hii kwa
Amani, Upendo na Utulivu
tukidumisha Mshikamano
wa Kitaifa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA**

Heri ya

# Mwaka Mpya

# 2026

www.singida.go.tz singidars

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA

SALAMU ZA MWAKA MPYA

## 2026

Mimi **Halima Dendego,** Mkuu wa Mkoa wa Singida ninaungana na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kuwatakia Heri ya Mwaka Mpya Wananchi wote wa Mkoa wa Singida.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida iko pamoja nanyi.
Tunasikiliza sauti zenu, tunaelewa mahitaji yenu, na tunachukua hatua mahususi za maboresho ya huduma katika sekta zote tunazotekeleza ili kuwahudumia wadau kwa UTU na heshima.

Tunaendelea kulinda amani, kuimarisha umoja na kujenga kwa vitendo mustakabali wa matumaini ya Taifa letu.

#Tunasikiliza
#TunajengaMustakabaliMpyaWaMatumaini
#TunasongaMbelePamoja



**MHE. HALIMA DENDEGO**

MKUU WA MKOA WA SINGIDA

SALAMU ZA MWAKA MPYA

## 2026

Mimi **Dkt. Fatuma Mganga,** Katibu Tawala Mkoa wa Singida, ninaungana na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kuwatakia Heri ya Mwaka Mpya Wananchi wote wa Mkoa wa Singida.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida iko pamoja nanyi.
Tunasikiliza sauti zenu, tunaelewa mahitaji yenu, na tunachukua hatua mahususi za maboresho ya huduma katika sekta zote tunazotekeleza ili kuwahudumia wadau kwa UTU na heshima.

Tunaendelea kulinda amani, kuimarisha umoja na kujenga kwa vitendo mustakabali wa matumaini ya Taifa letu.

#Tunasikiliza
#TunajengaMustakabaliMpyaWaMatumaini
#TunasongaMbelePamoja



**DKT. FATUMA MGANGA**

KATIBU TAWALA MKOA WA SINGIDA

# SINGIDA YETU

**NURU YA MAENDELEO**

*JARIDA MAALUM LA OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA*

TOLEO LA DESEMBA **2025**

**Jarida hili limetolewa na**
**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida**
**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

"Tunachochea Mendeleo, Kupitia Taarifa Sahihi"

**www.singida.go.tz**

